# <u>Jinsi tulivyo</u>

## Mundia

*Nilifanya mahojiano na Mundia kwa Kiingereza, halafu matini haya yalitafsiriwa kwa Kiswahili.*

Ninaitwa Mundia na mimi ni mwanaLGBTQ kutoka Kenya. Utambulisho wangu wa kijinsia ni tata.



Nilielewa kwamba mimi ni mqueer nilipokuwa mtoto.
Sikujua maneno ya kueleza uzoefu wangu lakini nilijua ndiye mimi siye kama kila mtu mwingine. Niliambiwa na watoto wengine kwamba ninaongea kama msichana, lakini halikuwa tatizo kubwa – bado tulikuwa marafiki na nilikuwa mimi mwenyewe.
Nilijifunza maneno ya kueleza uzoefu na utambulisho wangu wakati wa shule ya sekondari. Wakati wa shule ya msingi nilikuwa mimi mwenyewe, lakini hali ilianza kuwa ngumu baada ya hapo. Nilipofika shule ya sekondari, nilikuwa peke yangu na watu walinidhihaki na waliniiga. Kulikuwa na wanaLGBTQ wengine katika shule yangu, na tulijuana, lakini hatukuwa marafiki. Shule ya sekondari yangu ilikuwa shule ya wavulana tu mjini Thika, mbali sana na nyumba yangu huko Voi. Nilikuwa nakosa nyumba yangu sana na nilijisikia mpweke. Kwenda huko ilikuwa mshtuko wa kitamaduni halafu kulikuwa na uonevu wa wanadarasa wenzangu. Hakuna mtu aliyetaka kukaa kando ya mimi mezani. Siku moja nilisimikwa kama mkuu wa darasa na mwalimu wangu. Ilikuwa changamoto na watu waliniita kipenzi cha mwalimu, kwa hiyo nilimwomba amsimike mtoto mwingine, lakini alikataa. Leo ninajua ndio marafiki mazuri ni nani, kwa hiyo sitaki kusema kwamba nilikuwa na marafiki mazuri kwenye shule ya sekondari – siku hizi hatuongei.
Wakati wa shule ya sekondari niliwazia kuhusu maisha yangu baada ya kumaliza shule. Nilifikiri kwamba nitakuwa huru, lakini sikuwa na muda mwingi wa kuyafikiria kwa sababu nilikuwa nikitumia nguvu zangu kwa kuendelea kudumu masiha ya kila siku katika shule ile.



Leo, marafiki zangu wote wanajua kwamba mimi ni mqueer. Sikuzote wamejua. Baada ya kumaliza shule ya sekondari, mara nyingi nilihudhuria matukio ya ubunifu wa mawazi na niliandika blogu kuhusu yao. Siku moja nilianza kwenda katika kilabu cha wanaLGBTQ kwenye Westlands (Nairobi), na hivyo nilikutana na marafiki zangu wazuri sana. Hapo ndio unaweza kukutana na watu ambao wana vibe sawa na wewe.

Familia yangu hawajui kwamba mimi ni mqueer. Kuna ndugu fulani wanaojua lakini familia ya karibu yangu  hawajui wote. Ninawatembelea mara nyingi na nikiwa hapo, ninajaribu kujifanya mpenzi wa jinsia tofauti. Lazima nipunguze uzito wa jinsi nilivyo. Bado ninasikia kwamba familia yangu wananipea faraja na wananismamia. Labda wachache wao wanashuku juu ya jinsia yangu lakini sijui...



Kama mwanaLGBTQ hapa Kenya ninajihisi nimezuiliwa katika kujionyesha na kuonwa na yule ambaye ninataka kuwa naye. Ninafikiri kwamba ni ninazuiliwa katika kazi yangu kama mwanamtindo, sipati kazi nyingi kwa sababu hakuna kazi nyingi kwa watu kama mimi. Ningependa sana Wakenya wawe na uwazi wa kififikra zaidi, waache kujali nini tunachofanya na watupe fursa ya kuishi maisha yetu.

Bado sijasikia kwamba sheria za Kenya hainizuii kuwa mimi mwenyewe. Kama ninataka kujipodoa, nitajipodoa. Kama ninataka kwenda shereheni, nitapanda teksi badala ya matatu. Hiyo ni kwa sababu ninataka kuwa salama na pia ninataka kulinda nguvu yangu. Huko Westlands watu wanajishughulisha na mambo yao wenyewe, hawatatoa hukumu kuhusu nguo ninazozivaa.



Kitu ninachokipenda zaidi kuhusu kuwa mwanaLGBTQ ni kwamba kuna upendo mwingi sana. Ninauhisi katika kila mahali ya wanaqueer ninapoenda. Kwa mfano, majuzi nilikwenda katika sherehe ya pride, na nilijibamba sana.

Jambo ambalo ningependa watu wengi zaidi waelewe kuhusu jinsia yangu ni kwamba ni sehemu ndogo ya nafsi yangu – hainifafanui. Inafafanua tu mtu ambaye ninataka kufanya mapenzi naye, lakini sio utu wangu.



## Masai

*Nilimtumia Masai maswali kuhusu jinsia yake kwa Kiswahili na Kiingereza. Aliamua kujibu kwa Kiingereza, lakini nimetafsiri vitu alivyoviandika kwa Kiswahili.*

Ninaitwa Masai, ninaishi Nairobi. Mimi ni gay, pia utambulisho wa kijinsia wangu ni tata. Ninafanya kazi katika majengo yenye maduka kama msanii wa mapambo. Marafiki zangu walio wengi ni waqueer, na marafiki zangu ambao ni watu wenye jinsia mbalimbali wanajua kwamba mimi ni mqueer. Familia yangu hawajui kuhusu jinsia yangu, lakini ninafikiri pengine wanashuku juu yake. Kukua kama mtoto mqueer katika mazingira yanayochukia wanaLGBTQ ilikuwa ngumu, lakini nilijifunza kutanguliza afya na usalama wangu. Ni kitu cha ajabu kwamba kuwa mwanaLGBTQ ni kitu kipya kwa watu walio wengi Kenya. Lakini kadiri muda unavyopita, watu wanaanza kuwa wavumilivu zaidi. Sheria za Kenya zinazoharamisha uhalifu kuwa mwanaLGBTQ zinaweza kuzuia waqueer kuwa wao wenyewe. Watu wengi wanasema kuwa mwanaLGBTQ sio mtu wa kawaida na wanatumia dhana hiyo kusambaza chuki na ubaguzi wao.



Kitu ninachokipenda zaidi kuhusu kuwa mwanaLGBTQ ni kwamba ninaweza kuchagua familia yangu. Ningependa sana watu wengi zaidi waelewe kwamba ujinsia ni spektra.



## Machila

Ninaitwa Machila na ninaishi Nairobi. Mimi ni shoga na wa jinsia ya kiume, ninahisi kwamba nimeunganisha na wanaume kihisia. Tangu utotoni nilijua kwamba mimi ni mwanaLGBTQ. Nilianza kufind men attractive then.



Marafiki zangu wanajua kwamba mimi ni gay. Lakini sio wote. Kuna wengine bado siwaamini vizuri. Lakini kuna wale ambao ni marafiki zangu wa dhati, hao wanajua. Niliwaambia pindi nilipojiunga na chuo kikuu. Familia yangu hawajui kwamba mimi ni gay. Kuwa mtoto mqueer ilikuwa ngumu kwa kweli. Wengi walisema mimi ni kijana msichana. I had a touch of femme I couldn't  hide, waliniaibisha. Kwa sasa niko sawa kuishi Kenya kama mwanaLGBTQ. Nafeel limited lakini niko na imani mambo yatabadilika. Siskii kwamba sheria zinazokataza kuwa na uhusiano kiqueer zinakuzuia kuishi kwa uhuru. Sheria imeandikwa lakini serikali haiitekelezi kikamilifu. Serikali inamind its business. Kuwa gay ni baraka. Being gay has taken me place I don't think I would have gone kama ningekuwa straight. Kuwa gay ni furaha, tuko huru, tunajieleza kabisa. Ningependa watu wengi zaidi waelewe kuhusu jinsia yangu kwamba sio kitu kikubwa. Tafadhali tujifunze kuruhusu watu kupenda wanaotaka kupenda? Watu waachane na mambo ya watu wengine.



Picha zote katika makala haya ni zangu. Ninazichapisha na idhini ya wahusika wote.

All pictures in this article are mine. I upload them with the approval of all people depicted.